MWONGOZO WA MFUMO

# Mfumo mmoja unaoendesha hospitali nzima — kutoka mapokezi hadi ripoti ya wizara.

Umeandaliwa kwa hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati. Kila skrini kwenye kitabu hiki ni picha halisi ya mfumo ukifanya kazi, siyo mchoro wa kubuni.

**141**
skrini za kazi

**23**
makundi ya huduma

**553**
njia za API

**2**
lugha: Kiswahili / English

# Yaliyomo


1. Kwa nini mfumo huu
Tatizo linalotatuliwa

2. Mfumo kwa muhtasari
Muundo na sehemu zake

3. Safari ya mgonjwa
Hatua 10, mwanzo mwisho

4. Idara kwa idara
Kila kitengo na skrini zake

5. Fedha na uwajibikaji
Pesa haipotei kimya kimya

6. Hospitali kubwa na zahanati
Mfumo mmoja, saizi mbili

7. Usalama na kumbukumbu
Nani aliona, nani alibadilisha

8. Ripoti na bima
HMIS, IDSR, NHIF

9. Simu na kompyuta binafsi
API iliyoandikwa kikamilifu

10. Kuanza: nini kinahitajika
Vifaa, mtandao, mafunzo

11. Yasiyokuwepo bado
Tunachosema wazi

12. Maswali ya kawaida
Majibu mafupi

13. Kiambatisho: skrini zote
Picha za skrini zote

01

# Kwa nini mfumo huu

Hospitali nyingi zinaendeshwa kwa madaftari matano yasiyoongea: daftari la mapokezi, la maabara, la famasia, la mahesabu, na la wafanyakazi. Mgonjwa mmoja anaandikwa mara tano, na mwisho wa mwezi hakuna mtu anayejua kwa uhakika ni kiasi gani kilipatikana, ni dawa ngapi zimetoka, wala ni wagonjwa wangapi hawakurudi.

◉

### Kuandika mara moja

Mgonjwa anasajiliwa mara moja tu. Maabara, famasia, wodi na uhasibu wote wanasoma faili moja — hakuna kuandika upya wala majina yanayotofautiana.

₮

### Kila senti inafuatiliwa

Huduma inayotolewa inatengeneza ankara; malipo yanatengeneza risiti; vyote vinaingia kwenye leja. Hakuna njia ya pili ya kupokea fedha.

◔

### Foleni inayoonekana

Uongozi unaona kwa wakati halisi ni wagonjwa wangapi wanasubiri, wanasubiri kwa muda gani, na wamekwama wapi.

▣

### Ripoti bila kukesha

Ripoti za HMIS na ufuatiliaji wa magonjwa zinatoka kwenye kazi ya kila siku, siyo kwa kupiga hesabu za madaftari usiku wa kuamkia tarehe ya mwisho.

✓

### Kila kitendo kina jina

Nani alifuta ankara, nani alitoa punguzo, nani alitoa dawa — kumbukumbu inaandikwa na seva yenyewe, na haiwezi kufutwa na mtumiaji.

⇄

### Kiswahili na Kiingereza

Menyu na maelekezo yapo kwa lugha zote mbili. Mfanyakazi anachagua lugha yake mwenyewe; rekodi za kitabibu zinabaki Kiingereza kama zilivyo kwenye fomu za taifa.

02

# Mfumo kwa muhtasari

Sehemu zote zinazoonekana hapa zinaishi kwenye seva moja ya hospitali. Wafanyakazi wanaingia kwa kivinjari; simu na kompyuta binafsi zinatumia lango lilelile.




Lango moja tu ndilo linalofunguliwa nje. Kila ombi linapita hapo, linathibitishwa, na linaandikwa kwenye kumbukumbu — hakuna njia ya kando ya kufikia rekodi.




**Dashibodi ya siku**

Kila kitengo kwa mtazamo mmoja: waliopokelewa, wanaosubiri daktari, vitanda, vipimo, dawa zilizopungua, na fedha za siku.

03

# Safari ya mgonjwa, mwanzo mwisho

Hatua kumi kutoka mlangoni hadi rekodi ya mwisho. Kila hatua inaonyesha kile mfanyakazi anachofanya, na kile mfumo unachozuia kisitokee.



## 1 Mapokezi: kusajili au kumtambua anayerudi

Mgonjwa mpya anasajiliwa kwa fomu moja: jina, jinsia, umri, simu, mkoa, ndugu wa karibu, na bima kama anayo. Mfumo unatoa namba ya faili (MRN) mwenyewe. Anayerudi anatafutwa kwa jina, namba ya simu au namba ya faili — halisajiliwi upya.

> **Kinachozuiliwa:** namba ya taifa iliyotumika tayari inakataliwa na daftari, hivyo mtu mmoja hawezi kuishia na faili mbili.




Usajili mpya




Daftari la wagonjwa wote

## 2 Ada ya faili na ya daktari

Hospitali inaweka ada zake yenyewe kwenye orodha ya bei. Ikiwa imechaguliwa kukusanya kabla ya kuonana na daktari, mgonjwa analipa mapokezi na risiti inatoka papo hapo. Mwenye bima haulizwi fedha — dai linatengenezwa badala yake.




Orodha ya bei




Mtiririko wa mgonjwa

## 3 Foleni: kila mtu anajua zamu yake

Bodi ya foleni inaonyesha namba na kituo. Wauguzi na madaktari wanaona orodha ileile: nani anasubiri, amesubiri dakika ngapi, na yupo hatua gani.




Bodi ya foleni (ukumbi wa kusubiri)




Mahudhurio ya leo

## 4 Triage: vipimo vya awali

Muuguzi anapima joto, shinikizo la damu, mapigo, uzito na kiwango cha oksijeni. Vipimo hivi vinabaki kwenye faili la mgonjwa milele, na daktari anaviona kabla hajaanza.

> **Kinachozuiliwa:** kupima si kuandika matibabu. Muuguzi wa triage hawezi kuandika uchunguzi wa daktari, na daktari hahitaji ruhusa ya ziada kupima.




Uchambuzi wa awali

## 5 Chumba cha daktari

Daktari anaandika historia, uchunguzi, utambuzi na mpango wa matibabu. Kutoka skrini hiyohiyo anaagiza vipimo, anaandika dawa, anampa rufaa au anamlaza.




Foleni ya daktari




Uchunguzi na maelezo

## 6 Maabara na picha

Agizo linafika maabara likiwa na jina, namba ya faili na sababu. Mtaalamu anaingiza majibu; majibu yanayovuka mipaka hatarishi yanawekwa kwenye orodha ya dharura ili mtu aone na kuthibitisha kuwa ameyaona.

> **Macho mawili:** aliyeingiza majibu hawezi kuwa ndiye anayeyaidhinisha. Mfumo unakataa, hata kama mtu ana ruhusa zote mbili.




Maagizo ya maabara




Majibu na uthibitisho

## 7 Famasia: dawa zinatoka kwenye rafu na kwenye hesabu

Mfamasia anaona agizo la daktari, anatoa dawa, na hifadhi inapungua kwenye mfumo wakati uleule. Betchi na tarehe ya mwisho wa matumizi vinafuatiliwa, na dawa zinazokaribia kwisha muda zinaonekana mapema.




Maagizo ya dawa




Hifadhi ya dawa

## 8 Kulazwa: wodi, kitanda na chati

Mgonjwa anapangiwa kitanda halisi kwenye wodi halisi. Kazi za uuguzi na dozi za dawa zinapangwa kwa saa, na gharama ya kitanda inaingia kwenye ankara kila usiku bila mtu kukumbushwa.




Waliolazwa




Kituo cha wauguzi

## 9 Ankara, risiti na bima

Kila huduma iliyotolewa inaingia kwenye ankara moja ya mgonjwa. Mhasibu anapokea fedha — taslimu, simu au kadi — na risiti inachapishwa. Kwa mwenye bima, dai linaandaliwa kwa mfuko wake pamoja na asilimia inayogharamiwa.




Kaunta ya malipo


Hospitali ya Wilaya ...
Hospital · Ngazi 5
Tafuta wagonjwa, ankara, vipimo...
Mtandaoni
Hospitali ya Wilaya ya Mfano
Muhtasari
Mapokezi
Wagonjwa
Mahudhurio
Kliniki
Afya ya Mama na Mt...
Kliniki Maalum
Chumba cha Upasuaji
Uchunguzi
Famasia na Ghala
Wagonjwa wa Kulaz...
Fedha
Ankara
Ankara Zote
Madeni
Mhasibu
Risiti
Makusanyo
Wagonjwa wa Bima
Madai ya Bima
Bei za Huduma
Matumizi
Taasisi
admin
SYSTEM_ADMIN
Bills
Everything charged, and what is left to collect.
Raise a bill
Billed today
TSh 116,000
Collected today
TSh 68,500
Outstanding
TSh 47,500
12 bills
With schemes
TSh 0
0 claims
Search by patient, number or bill...
Status All Payer All
BILL PATIENT PAYER TOTAL OWING STATUS
INV-000016 08 Sep 2026 Zainabu Mushi MRN-000031 cash TSh 17,000 TSh 8,500 PARTIAL Invoice
INV-000014 08 Sep 2026 Amina Mwakyusa MRN-000029 cash TSh 13,000 TSh 13,000 ISSUED Invoice
INV-000012 08 Sep 2026 Mwajuma Ngowi MRN-000035 cash TSh 5,000 TSh 0 Paid Invoice
INV-000010 08 Sep 2026 Daniel Lyimo MRN-000038 cash TSh 13,000 TSh 0 Paid Invoice
INV-20260908-00013 08 Sep 2026 Joseph Mrema MRN-000034 insurance TSh 0 TSh 0 ISSUED Invoice
INV-20260908-00012 08 Sep 2026 Halima Massawe MRN-000033 insurance TSh 0 TSh 0 ISSUED Invoice
INV-20260908-00011 08 Sep 2026 Baraka Kimaro MRN-000030 insurance TSh 0 TSh 0 ISSUED Invoice
INV-20260908-00010 08 Sep 2026 Emmanuel Macha MRN-000044 cash TSh 0 TSh 0 ISSUED Invoice
INV-20260908-00009 08 Sep 2026 Zainabu Temu MRN-000043 cash TSh 0 TSh 0 ISSUED Invoice

Ankara zote

## 10 Kufunga faili na kutoa ripoti

Mahudhurio yanafungwa yakiwa na utambuzi na matokeo. Kumbukumbu za matibabu zinapangwa kwa msimbo, na takwimu za HMIS zinajijenga kutoka kwenye kazi iliyofanyika — siyo kutoka kwenye kuhesabu madaftari mwisho wa mwezi.




Kumbukumbu za matibabu




Ripoti za HMIS

04

# Idara kwa idara

Zaidi ya safari ya mgonjwa, mfumo unashika kila kitengo kinachoendesha hospitali. Hapa ni muhtasari; skrini zote 141 zipo kwenye kiambatisho mwishoni.

## Dharura na ajali

Waliofika kwa dharura wanaandikwa hata kama hawajulikani kwa jina, wanapangwa madaraja matano ya uzito, na bodi inaonyesha nani anahitaji kuonwa sasa hivi.




Dharura na ajali

## Afya ya mama na mtoto

Kliniki ya ujauzito, uchungu na kujifungua, huduma baada ya kujifungua, uzazi wa mpango, chanjo na ufuatiliaji wa ukuaji. Kila huduma hapa ni ratiba ambayo mtu anaweza kuikosa — hivyo kila orodha ina kichujio cha "waliochelewa".




Kliniki ya ujauzito




Chanjo (EPI)

## Kliniki za programu

Kifua kikuu, tiba na matunzo ya VVU, na magonjwa sugu yasiyoambukiza. Kila mgonjwa ana kundi, hatua ya matibabu, na tarehe ya kurudi — na wasiorudi wanaonekana kwenye orodha moja badala ya ripoti mtu anayopaswa kukumbuka kuiendesha.




Kliniki ya kifua kikuu

## Chumba cha upasuaji

Ratiba ya vyumba, timu ya upasuaji, orodha ya ukaguzi wa usalama, na hesabu ya vifaa vilivyoingia na kutoka. Upasuaji haufungwi kama hesabu hazilingani — na hilo si suala la cheo cha mtu, ni kanuni ya mfumo.




Chumba cha upasuaji

## Ghala, manunuzi na wasambazaji

Kutoka oda ya manunuzi, hadi kupokea mzigo, hadi ankara ya msambazaji, hadi malipo. Hatua nne, watu tofauti — ndiyo maana msambazaji hawezi kulipwa kwa mzigo ambao haujawahi kufika.




Bidhaa na dawa




Manunuzi

# Rasilimali watu na mishahara

Waajiriwa, nafasi za kazi, mahudhurio ya kazi, likizo, ajira mpya, mafunzo, nyaraka za mfanyakazi, na mishahara. Mishahara ina hatua tatu: kuandaa, kuhesabu, na kuidhinisha — na aliyeandaa si anayeidhinisha.




Waajiriwa




Mishahara

# Huduma saidizi

Benki ya damu, chumba cha maiti, magari ya wagonjwa, na mali na matengenezo. Kila kimoja kinawashwa tu kwenye tawi lenye huduma hiyo.




Benki ya damu




Mali na matengenezo

05

# Fedha na uwajibikaji

Sehemu ngumu zaidi ya hospitali si kutibu — ni kuhakikisha kile kilichotolewa kimelipiwa, na kile kilicholipwa kimeingia benki. Mfumo huu unashika hatua zote kwenye njia moja.




Hakuna njia ya pili ya kupokea fedha — kila senti inapita hapa.
There is no second till: every shilling passes along this line.

## Vidhibiti vilivyojengwa ndani

| KITENDO | NANI ANARUHUSIWA | KWA NINI |
|---|---|---|
| Kutoa punguzo kwenye ankara | Ruhusa yake pekee | Punguzo ni njia halali ya fedha kutoka — na pia njia isiyo halali. |
| Kufuta ankara | Ruhusa nyingine tofauti | Aliyeitengeneza ankara asiwe ndiye anayeifuta. |
| Kurudisha malipo | Ruhusa ya juu kabisa ya kaunta | Ni fedha inayotoka mkononi baada ya kuingia. |
| Kubadilisha kuingizwa kwenye leja | Hairuhusiwi kwa mtu yeyote | Kosa linarekebishwa kwa kuingiza kinyume chake, ili historia ibaki. |
| Kuchapisha noti ya krediti | Ankara iliyolipwa pekee | Noti ya krediti dhidi ya deni hai ni hati ya uongo. |
| Kulipa msambazaji | Baada ya oda, risiti ya mzigo na ankara kulingana | Hii ndiyo inayozuia malipo ya mzigo usiokuwepo. |




Jarida na leja




Taarifa za fedha




Fedha zilizopo mkononi




Madeni ambayo hayajalipwa

> **Hati zinazochapishwa:** ankara, risiti, noti ya krediti, taarifa ya mgonjwa, vocha ya matumizi, oda ya manunuzi, hati ya malipo kwa msambazaji, na slipu ya mshahara — zote zinatoka kwenye mfumo zikiwa na jina, nembo na anwani ya hospitali.

06

# Hospitali kubwa na zahanati ndogo

Mfumo ni mmoja. Kinachotofautiana ni kile kilichowashwa kwenye kila tawi. Zahanati isiyo na chumba cha upasuaji haioni menyu ya upasuaji hata kidogo — na wala haiwezi kufungua ukurasa huo kwa kuandika anwani yake.

**Hospitali ya wilaya · District hospital**

- ✓ Mapokezi, wagonjwa, mahudhurio
- ✓ Maabara na picha (X-ray, ultrasound)
- ✓ Wodi, kulazwa, chumba cha upasuaji
- ✓ Benki ya damu, chumba cha maiti
- ✓ Kliniki za TB na CTC, meno, macho
- ✓ Gari la wagonjwa, manunuzi, uhasibu kamili
- ✓ Rasilimali watu na mishahara

≈ 141 skrini zimewashwa

**Zahanati · Dispensary**

- ✓ Mapokezi, wagonjwa, mahudhurio
- ✓ Vipimo vya haraka (RDT, sukari)
- ✓ Famasia na ghala dogo
- ✓ Kliniki ya mama na mtoto, chanjo
- ✓ Malipo, risiti, madeni, ripoti za HMIS
- ✗ Chumba cha upasuaji — hakipo
- ✗ Benki ya damu, chumba cha maiti — havipo

≈ 60 skrini zimewashwa; nyingine zimefichwa

Kuwasha au kuzima ni kazi ya msimamizi, si ya fundi wa kompyuta. Inafanyika kwenye skrini moja, na sababu inaandikwa — ili mtu atakayeuliza "kwa nini menyu hii haipo?" apate jibu badala ya kukisia.




**Moduli na huduma — swichi za tawi** Zilizozimwa zinatoweka kwenye menyu ya kila mfanyakazi wa tawi hilo, na API inakataa maombi yake.

## Matawi mengi, mfumo mmoja

Hospitali yenye vituo vya kando inaviendesha vyote kwenye mfumo mmoja. Kila tawi linaona rekodi zake; uongozi wa juu unaona vyote kwa pamoja. Mfanyakazi anayehudumu tawi moja haoni fedha wala wagonjwa wa tawi jingine.


Hospitali ya Wilaya ...
Hospital · Ngazi 5
Tafuta wagonjwa, ankara, vipimo...
Ctrl K
Mtandaoni
Hospitali ya Wilaya ya Mfano
A
Muhtasari
Mapokezi
Wagonjwa
Mahudhurio
Kliniki
Afya ya Mama na Mt...
Kliniki Maalum
Chumba cha Upasuaji
Uchunguzi
Famasia na Ghala
Wagonjwa wa Kulaz...
Fedha
Taasisi
Wasifu wa Taasisi
Matawi
Idara
Ofisi na Maeneo
Wateja na CRM
Mauzo na POS
Rasilimali Watu
Fedha za Tawi
Uhasibu
admin
SYSTEM_ADMIN
Branches
Every site in the network, and the service tier each one runs at.
+ Add a branch
Branches
2
Active
2
Licensed beds
124
Hospitali ya Wilaya ya Mfano
Primary
Active
HQ
Hospital · level 5
Full inpatient, theatre, blood bank, mortuary and support services.
Kiboriloni, Moshi, Kilimanjaro
120 licensed beds · Public
You are working in this branch
Edit branch
Zahanati ya Kilimani
Active
ZK
Dispensary · level 1
Outpatient, RCH, basic laboratory and dispensing. Refers upward.
Kilimani, Moshi, Kilimanjaro
4 licensed beds · Public
16 modules switched off here
Edit branch

Matawi

07

# Usalama, ruhusa na kumbukumbu

Rekodi ya mgonjwa ni siri ya kisheria. Mfumo hauzuii tu kwa kuficha vitufe — seva yenyewe inakataa ombi la mtu asiye na ruhusa, hata kama ameandika anwani moja kwa moja.

### Ruhusa kwa kila kitendo

Zaidi ya ruhusa 160 tofauti. Mhasibu anaona fedha, si majibu ya maabara; muuguzi anaona chati, si mishahara.

### Kumbukumbu isiyofutika

Kila kitendo kinaandikwa na seva: nani, lini, kitu gani. Hakuna njia ya mtumiaji kuandika au kufuta kwenye kumbukumbu hiyo.

### Macho mawili

Majibu ya maabara, mishahara, matumizi na kurudisha fedha — vyote vina mtu wa kuandaa na mtu mwingine wa kuidhinisha.

### Akaunti za wafanyakazi

Hakuna kujisajili mwenyewe. Msimamizi ndiye anayefungua akaunti, anaipa majukumu, na anaweza kuisimamisha siku mfanyakazi anapoondoka.




Watumiaji na majukumu




Kumbukumbu za mfumo

**Kuhusu mtandao unapokatika:** mfumo hausemi uongo. Ukikatika, skrini inaonyesha wazi kuwa hakuna mtandao na kwamba kilichoandikwa hakitahifadhiwa — badala ya kuonyesha

> alama ya "imehifadhiwa" kwa kitu ambacho hakijafika seva.

---

08

# Ripoti za kitaifa na bima

Takwimu za HMIS zinajengwa kutoka kwenye mahudhurio, utambuzi na huduma zilizotolewa. Magonjwa ya kuarifiwa (IDSR) yanaandikwa yanapotokea, na yale ya dharura yanawekwa alama ya kuarifiwa mara moja.




**Ufuatiliaji wa magonjwa (IDSR)**




**Madai ya bima**

Kwa upande wa bima: mifuko inasajiliwa na asilimia yake ya ugharamiaji, dai linaandaliwa kutoka kwenye ankara halisi, na hatua zake zinafuatiliwa hadi linapolipwa au kukataliwa — pamoja na sababu.




**Takwimu za uendeshaji** Mwenendo wa wagonjwa, mapato, na muda wa kusubiri.

09

# Simu ya mkononi na kompyuta binafsi

Mfumo unafunguliwa kwa kivinjari kwenye kompyuta yoyote ya hospitali — hakuna programu ya kusakinisha kila mashine. Kwa wanaotaka app ya simu au programu ya desktop (kwa mfano kwa ajili ya printa za risiti au kisoma-bakodi), API yote imeandikwa kikamilifu: njia 553, pamoja na faili ya Postman na OpenAPI kwa watengenezaji.

### Wodi

Kupima vitals, kuona chati na kusonga foleni kwa kishikwambi.

### Kaunta

Programu ya desktop inayochapisha risiti moja kwa moja kwenye printa.

### Mgonjwa

Portal ya mgonjwa: miadi, majibu yaliyoruhusiwa, ankara na ujumbe.




**Skrini ya kuingia** Jina na nembo ya hospitali yenyewe, si ya muuzaji wa mfumo.

10

# Kuanza: nini kinahitajika

| KIPENGELE | ZAHANATI / KITUO CHA AFYA | HOSPITALI YA WILAYA |
|---|---|---|
| Seva | Kompyuta moja imara (8GB RAM) au seva ya wingu | Seva ya kweli (16GB+), au wingu |
| Kompyuta za watumiaji | 2 – 5 | 15 – 60 |
| Mtandao | LAN ya ndani; intaneti si lazima kwa kazi ya kila siku | LAN imara; intaneti kwa bima na ripoti |
| Umeme | UPS kwa seva | UPS na jenereta |
| Printa | Moja ya risiti | Risiti, ankara, na lebo |
| Mafunzo | Siku 2 | Siku 5 – 10, kwa vitengo |

## Hatua za usakinishaji

1. **Wiki 1 — Kuweka mfumo.** Seva, mtandao, na kuingiza wasifu wa hospitali: jina, nembo, matawi, idara, na orodha ya bei.
2. **Wiki 2 — Watumiaji na ruhusa.** Kufungua akaunti za wafanyakazi na kuwapa majukumu yanayolingana na kazi zao halisi.
3. **Wiki 3 — Mafunzo kwa vitengo.** Mapokezi na kaunta kwanza, kisha kliniki, maabara na famasia, mwisho uhasibu.
4. **Wiki 4 — Kuanza kwa hatua.** Kuanza na mapokezi na malipo pekee kwa siku chache, kisha kuongeza vitengo vingine hadi vyote viwe ndani.
5. **Kuendelea — Hifadhi nakala.** Nakala ya kila siku, na jaribio la kurejesha mara moja kwa mwezi. Hifadhi ambayo haijawahi kujaribiwa si hifadhi.

11

# Yasiyokuwepo bado

Tunayaeleza wazi, kwa sababu kugundua baadaye ni gharama kubwa zaidi kuliko kuambiwa mapema.

- **Risiti za kielektroniki za TRA (EFD).** Mfumo unachapisha risiti zake zenye namba na kumbukumbu kamili, lakini bado hauunganishwi moja kwa moja na mashine ya EFD.
- **Kutuma SMS.** Mfumo unaandaa ujumbe na kuuweka kwenye foleni, lakini hospitali inahitaji akaunti ya lango la SMS ili ujumbe utoke kweli.
- **Kufanya kazi bila mtandao kabisa.** Kompyuta lazima iwe imeunganishwa na seva ya hospitali. Ikikatika, mfumo unasema wazi badala ya kuhifadhi kimyakimya.
- **Vifaa vya maabara vinavyojiunganisha vyenyewe.** Majibu yanaingizwa na mtaalamu; muunganisho wa moja kwa moja na mashine ni kazi ya baadaye.

12

# Maswali yanayoulizwa mara kwa mara

### Je, tunaweza kuanza na vitengo vichache tu?

Ndiyo, na ndiyo njia inayoshauriwa. Anza na mapokezi na malipo; ongeza maabara, famasia na wodi mfululizo. Vilivyozimwa havionekani kabisa kwenye menyu.

### Rekodi zetu za zamani zitaingiaje?

Daftari la wagonjwa linaweza kuingizwa kwa faili (majina, namba za faili, simu, bima). Rekodi kamili za kitabibu za nyuma kwa kawaida hazihamishwi — hospitali huanza upya kwa wagonjwa wanaokuja, na daftari la zamani linabaki kama kumbukumbu.

### Data yetu inakaa wapi?

Kwenye seva ya hospitali yenu, au seva ya wingu mliyoichagua. Rekodi za wagonjwa hazitoki hapo — isipokuwa mkiamua wenyewe kuwasha msaada wa AI unaotumia huduma ya nje, ambao umezimwa mpaka mtakapouwasha na kuweka ufunguo wake.

### Umeme ukikatika wakati wa kazi?

Kilichohifadhiwa kimehifadhiwa. Kwa sababu kila kitendo kinatumwa seva mara moja, kilichopotea ni fomu iliyokuwa mkononi tu — siyo kazi ya siku nzima. UPS kwenye seva ndiyo kinga muhimu zaidi.

### Tunaweza kuona ni nani alifanya nini?

Ndiyo. Kila kitendo kina jina la aliyekifanya na saa. Kumbukumbu hiyo haiwezi kuhaririwa na mtumiaji yeyote, wa ngazi yoyote.

13

# Kiambatisho: skrini zote za mfumo

Picha zote zilizo hapa chini zilipigwa kwenye mfumo halisi ukiwa na data ya mfano ya hospitali ya kufikirika. Hakuna rekodi ya mgonjwa halisi iliyotumika.

## Muhtasari 2 skrini




### Dashibodi

Dashboard · /dashboard




### Bodi ya Foleni

Queue Board · /queue

## Mapokezi 4 skrini




### Usajili Mpya

New Registration · /reception/register




### Mgonjwa Anayerudi

Returning Patient · /reception/returning




## Miadi

Appointments · /appointments




## Foleni ya Mapokezi

Reception Queue · /reception/queue

---

# Wagonjwa 3 skrini




## Wagonjwa Wote

All Patients · /patients




## Sajili Mgonjwa

Register Patient · /patients/register




## Foleni ya Wagonjwa

Patient Queue · /patients/queue

---

# Mahudhurio 3 skrini




## Mahudhurio ya Leo

· /visits




## Mahudhurio Yanayoendelea

Active Visits · /visits/active




## Mahudhurio Yaliyokamilika

Completed Visits · /visits/completed

---

## **Kliniki** 7 skrini




## Foleni ya Daktari

Doctor Queue · /clinical/queue




## Uchambuzi wa Awali

Triage · /clinical/triage




## Uchunguzi

Consultation · /clinical/consultation




## Dharura na Ajali

Emergency & Casualty · /emergency




## Kituo cha Wauguzi

Nursing Station · /nursing




## Rufaa

Referrals · /referrals




## Kumbukumbu za Matibabu

Medical Records · /records

---

## Afya ya Mama na Mtoto 6 skrini



## Kliniki ya Ujauzito

Antenatal (ANC) · /rch/anc



## Uchungu na Kujifungua

Labour & Delivery · /rch/delivery



## Baada ya Kujifungua

Postnatal (PNC) · /rch/pnc



## Uzazi wa Mpango

Family Planning · /rch/family-planning



## Chanjo

Immunization (EPI) · /rch/immunization



## Ukuaji na Lishe

Growth & Nutrition · /rch/growth

---

## Kliniki Maalum 6 skrini




## Kliniki ya Kifua Kikuu

TB Clinic · /clinics/tb




## Kliniki ya Tiba na Matunzo

HIV Care & Treatment · /clinics/ctc




## Kliniki ya Magonjwa Sugu

NCD Clinic · /clinics/ncd




## Kliniki ya Meno

Dental Clinic · /clinics/dental




## Kliniki ya Macho

Eye Clinic · /clinics/eye




## Tiba ya Viungo

Physiotherapy · /clinics/physiotherapy

---

## Chumba cha Upasuaji 1 skrini



## Chumba cha Upasuaji

Operating Theatre · /theatre

---

## Uchunguzi 6 skrini



### Maagizo ya Maabara

Lab Orders · /laboratory/orders



### Vipimo Vinavyosubiri

Pending Tests · /laboratory/pending



### Majibu ya Maabara

Lab Results · /laboratory/results



### Maagizo ya Picha

Imaging Orders · /radiology/orders




## Majibu ya Picha

Imaging Results · /radiology/results




## Benki ya Damu

Blood Bank · /blood-bank

---

## Famasia na Ghala 9 skrini




## Maagizo ya Dawa

Prescriptions · /pharmacy/prescriptions




## Utoaji wa Dawa

Dispensing · /pharmacy/dispensing




## Hifadhi ya Dawa

Drug Stock · /pharmacy/inventory




## Bidhaa

Products · /inventory/products




## Leja ya Ghala

Stock Ledger · /inventory/stock




## Wasambazaji

Suppliers · /inventory/suppliers




## Maghala

Warehouses · /inventory/warehouses




## Mienendo ya Bidhaa

Stock Movements · /inventory/movements




## Manunuzi

Procurement · /procurement

---

## Wagonjwa wa Kulazwa 4 skrini



## Kulazwa

Admissions · /inpatient/admissions



## Wodi na Vitanda

Wards & Beds · /inpatient/wards



## Kuruhusiwa

Discharge · /inpatient/discharge



## Chumba cha Maiti

Mortuary · /mortuary

---

# **Fedha** 10 skrini



## Ankara

Bills · /billing



## Ankara Zote

Invoices · /billing/invoices




## Madeni

Outstanding · /billing/outstanding




## Mhasibu

Cashier · /cashier




## Risiti

Receipts · /cashier/receipts




## Makusanyo

Collections · /cashier/collections




## Wagonjwa wa Bima

Insured Patients · /insurance/patients




## Madai ya Bima

Claims · /insurance/claims




## Bei za Huduma

Service Tariffs · /finance/tariffs




## Matumizi

Expenses · /finance/expenses

---

## Taasisi 4 skrini




## Wasifu wa Taasisi

Company Profile · /organization




## Matawi

Branches · /facilities




## Idara

Departments · /organization/departments




## Ofisi na Maeneo

Offices & Locations · /organization/locations

---

## Wateja na CRM 3 skrini




## Wateja

Clients · /crm/clients




## Anwani za Wateja

Contacts · /crm/contacts




## Ufuatiliaji

Follow-ups · /crm/follow-ups

---

## Mauzo na POS  5 skrini




## Kituo cha Mauzo

Point of Sale · /sales/pos




## Nukuu za Bei

Quotations · /sales/quotations




## Oda za Mauzo

Sales Orders · /sales/orders




## Marejesho na Krediti

Returns & Credits · /sales/returns




## Kanuni za Punguzo

Discount Rules · /sales/discounts

---

## Rasilimali Watu 20 skrini




## Muhtasari wa Rasilimali Watu

HR Overview · /hr




## Waajiriwa

Employees · /hr/employees




## Idara za Utumishi

Departments · /hr/departments




## Nafasi za Kazi

Positions & Job Grades · /hr/positions




## Ajira Mpya

Recruitment · /hr/recruitment




## Kuanzisha Mfanyakazi

Onboarding · /hr/onboarding




## Mahudhurio ya Kazi

Attendance · /hr/attendance




## Likizo

Leave Management · /hr/leave



## Ratiba na Likizo

Roster · /staff/roster



## Mishahara

Payroll · /hr/payroll



## Marupurupu na Makato

Benefits & Deductions · /hr/benefits



## Utendaji

Performance Management · /hr/performance



## Mafunzo na CPD

Training & Development · /hr/training



## Mikataba

Employee Contracts · /hr/contracts




## Nyaraka za Wafanyakazi

Employee Documents · /hr/documents




## Nidhamu

Disciplinary Management · /hr/disciplinary




## Vifaa vya Wafanyakazi

Employee Assets · /hr/assets




## Kuondoka Kazini

Offboarding / Exit · /hr/offboarding




## Ripoti za Utumishi

HR Reports · /hr/reports




## Mipangilio ya Utumishi

HR Settings · /hr/settings

---

**Fedha za Tawi** 8 skrini




# Dashibodi ya Fedha

Dashboard · /accounts




# Akaunti za Fedha

Funding Accounts · /accounts/funding




# Uhamisho wa Fedha

Transfers · /accounts/transfers




# Kuweka Fedha

Deposits · /accounts/deposits




# Kutoa Fedha

Withdrawals · /accounts/withdrawals




# Miamala Yote

Transactions · /accounts/transactions




## Matumizi

Expenses · /finance/expenses




## Upatanisho

Reconciliation · /accounting/banking

---

## Uhasibu 11 skrini




## Muhtasari wa Uhasibu

Accounting Overview · /accounting




## Muhtasari wa Hesabu

Summary · /accounting/summary




## Jarida na Leja

Journals & Ledger · /accounting/journal




## Chati ya Akaunti

Chart of Accounts · /accounting/accounts




## Madeni Tunayodai

Receivables · /accounting/receivables




## Madeni Tunayodaiwa

Payables · /accounting/payables




## Benki na Fedha

Bank & Cash · /accounting/banking




## Taarifa za Fedha

Financial Statements · /accounting/statements




## Bajeti

Budgets · /accounting/budgets




## Kodi na Michango

Tax & Statutory · /accounting/tax




## Afya ya Uandishi

Posting Health · /accounting/posting-health

---

## Huduma Saidizi 2 skrini




## Gari la Wagonjwa

Ambulance & Fleet · /ambulance




## Mali na Matengenezo

Assets & Maintenance · /assets

---

## Nyaraka 1 skrini




## Daftari la Nyaraka

Document Register · /documents

## Ripoti 4 skrini




### Takwimu

Analytics · /analytics




### Ripoti za Uendeshaji

Operational Reports · /reports




### Ripoti za HMIS

HMIS Returns · /reports/hmis




### Ufuatiliaji wa Magonjwa

Disease Surveillance · /reports/idsr

## Utawala 22 skrini




### Orodha ya Wafanyakazi

Staff Directory · /staff




### Watumiaji na Majukumu

Users & Roles · /users




## Mawasiliano

Communications · /communications




## Matangazo

Announcements · /announcements




## Hifadhi Nakala

Backup & Restore · /settings/backup




## Muunganisho wa Mifumo

Integrations · /settings/integrations




## Maoni ya Wagonjwa

Patient Feedback · /feedback




## Kumbukumbu za Mfumo

Audit Log · /audit



## Wasifu wa Kituo

Facility Profile · /settings



## Mipangilio ya Mfumo

System Settings · /settings/system



## Mtiririko wa Mgonjwa

Patient Flow · /settings/patient-flow



## Mipangilio ya Uhasibu

Accounting Settings · /settings/accounting



## Mipangilio ya Bidhaa

Product Settings · /settings/products



## Moduli na Huduma

Modules & Services · /settings/modules




## Muonekano

Appearance · /settings/appearance




## Huduma za Mfumo

System Services · /settings/services




## Magari ya Wagonjwa

Ambulances · /settings/ambulance




## Arifa

Notifications · /notifications




## Idhini Zangu

My Approvals · /approvals




## Ujumbe

Messages · /messages




## Msaada wa Kiufundi

IT Helpdesk · /helpdesk




## Msaada

Help & Shortcuts · /help

---

**Kuingia** 1 skrini




## Kuingia kwenye mfumo

Sign in · /login

**Hospitali ya Wilaya ya Mfano** ni hospitali ya kufikirika iliyotumika kuandaa kitabu hiki. Majina, namba za simu, ankara na majibu yote ni ya kubuni.

Mwongozo huu unaambatana na nyaraka za API kwa watengenezaji (docs/api) kwa yeyote anayetaka kuunganisha mfumo mwingine au kujenga app.